


JANGA

(Diwani ya mashairi)



•ASIA •EUROPE •AFRICA •AMERICA

ALI SALIM MASITO (MUDIRI)

**Kimechapishwa na Destiny Ink Publishers
Ltd**

**Destiny Ink Publishers Ltd,
Barabara ya Kangundo,
S.L.P 39 Machakos,
Kenya.**

© Ali Salim Masito, 2024.

**Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga,
kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kutoa
kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini,
kwa maandishi ya Destiny Ink Publishers
Ltd.**

**Toleo la kwanza 2024,
ISBN: 978-9914-9811-0-0**

KIMO

Kuandikwa liandikwe, uwenda likawa
somo
La kuchekwa nalichekwe, nali bado mumo
humo
Lianike lianikwe, lisichafuwe mdomo
Hatutotizama kimo, wakurukwa na
arukwe

Lishikwalo nalishikwe, lisende tezi na
omo
La kuzamishwa lizukwe, pa chomo tupige
chomo
Msirika asirikwe, ya ndani iambwe imo
Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Iwe ni kando ya fukwe, hapo tupaweke
limo
Maji chumvi iwe kwekwe, tuburuge kwa
kilimo
Anyakaye na anyakwe, asiponyakwa mi
simo
Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Panapotaka patakwe, usimame msimamo
Waalika waalikwe, wahadharishwe na
shimo

Parukikapo parukwe, pasiwachwe na
lalamo

Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Kiekacho nakiekwe, kisitupige tutumo
Lekwe nayo nailekwe, ufupi wa eskimo
Simtusi mama mkwe, mana huwezi
vipimo

Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Kusumbuka pasumbukwe, iishe yao
nderemo

Kila mtu chake chakwe, yalivyo ndo
yaliyomo

Wamakaji nawamakwe, na tuwapige
mfano

Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Msisubiri nizekwe, mkazuwa yasiyomo
Kama fumbo lifumbikwe, waja
wang'amue somo

Ima hadi pazeekwe, zitolewe zilo mumo
Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

Mwisho hili liandikwe, tama yakwe hini
kimo

Mi mcheshi nisichekwe, kutojua
mungurumo

Wafunzaji wapulikwe, wanijuze yaliyomo
Hatutotizama kimo, wakuruka na arukwe

WAZAZI

Sinyamazi nalisema, kaniwezesha Azizi
Tena nalisema wima, nayataka masikizi
Lengo kuuhasa umma, na mambo ya siku
hizi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Baba simwachie mama, kumlimbikia kazi
Mwana kuwa na heshima, ataka mema
malezi
Si hivyo mkiterema, mwaja kufuga jiizi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Mumleavyo ni dhima, kesho mbele ya
Mwenyezi
Lisiwafike zahama, mtakapofumba ozi
Si kumfunza magoma, na mengi ya upuuzi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Jukumu lenu fahama, muyachuje
maongezi

Wafundeni vya salama, sio mawi na
manyenzi
Adabu watazichuma, wawe kesho
viongozi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Sio sukuma sukuma, hisia hamuulizi
Watambuweni mapema, msiwapuze
mapuzi
Na msiwaache nyuma, wafanyapo
maamuzi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Wasomesheni kusoma, kila watakayo kozi
Isiwe Baba kusema, na mama hakukatazi
Haiwi ulelemama, kwenda yao machaguzi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Msipeane lawama, mukatengana wazazi
Kwa malezi yalo mema, mwana hawi gozi
gozi

Hukuwa ja chanda chema, na akawa
msikizi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

Mudiri hapa nakwima, utungo siendelezi
Nimekumbusha gojama, mana kimya
sikiwezi
Na Mola wetu Karima, atatupa utatuzi
Shikamaneni wazazi, muwalee wana
vyema!

UKO WAPI BABA

Kwa uwezo wa karima, hii tungo yako
baba

Natumai umzima, popote ulipo baba
Tafuto lisilo koma, ninakutafuta baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Siachi kushika tama, kukufikiria baba
Moyoni linaniuma, lini takuona baba
Mwili unanitetema, ninakutamani baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Mwili unanizizima, sina jibu lako baba
Anavyoteseka mama, heri ugejua baba
Kama ulipo wahema, urudi nyumbani
baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Maswali ya tangu zama, mama
keshachoka baba
Ubaki kunitizama, nikumuuliza baba

Hana tena cha kusema, yanisikitisha baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Kama kosa rudi nyuma, msamehe mama
baba
Usizijali tuhuma, yasahau ewe baba
Akupenda wangu mama, naamini hilo
baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Mwanao mie nasoma, kimateso ewe baba
Sijui kuila nyama, pia fomu sina baba
Bidii ya wangu mama, ni tamaa yangu
baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Takupa yako heshima, daima u wangu
baba
Ila sifanye dhuluma, ulipo itika baba
Njoo mfariji mama, maisha magumu baba

Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

Tamati siachi tama, huzuni moyoni baba
Usingojee kiama, masuula uwe baba
Baba mrudie mama, tufurahikeni baba
Hana jibu tena mama, kwani uko wapi
baba

KOSA LA MWANA

Yeye

Hodi kwa Ali Masito, ninalo jambo

chukiza

Kukicha lapamba moto, kukitwa hutanda

Giza

Lishanizidi uzito, fafanuzi nauliza

Mbona akosapo mwana, alaumiwaye

mama

Mimi

Karibu Thuma Pereto, ulosema mesikiza

Mda mwingi na watoto, mama aweza

tuliza

Iweje mwana ni soto, mama kipi kapitiza

Kuharibika kwa mwana, kashifa ni zake

mama

Yeye

Mtoto kuwa msoto, sio mama kupoteza

Kuna mengi we Masito, na huko

anakocheza

Mwana kienda kushoto, baba pia

huchangiza

Mbona akosapo mwana, kosa hurushiwa
mama

Mimi

Baba na chake kikoto, mwana vyema
hupacheza
Huogopa mkong'oto, na mawi kujikataza
Heshima huweka nzito, baba akishatokeza
Kuharibika kwa mwana, ni uzembe wake
mama

Yeye

Siengemee kushoto, na kulia patiliza
Shuleni kipata mwito, baba mwana
meongoza
Munageuza mvuto, mwanao kakuigiza
Anapoteleza mwana,iweje atajwe mama

Mimi

Mama kwa yale mapito, mwana
hum'bembeleza
Haramu kushika fito, kumrudi uyapuza
Hata kumpiga ngoto, asema amuumiza

Kuharibika kwa mwana, ni makosa yake
mama

Yeye
Sioni kupiga ngoto, ndo mwana
kumuongoza
Au kucharaza fito, moja mbili fululiza
Mwana kulia na mto, si funzo wamuumiza
Hivi kipotea mwana, lawama liwe la
mama

Mimi
Walisema kina Dotto, kuchapa si kuumiza
Mwisho yabaki majuto, ya fimbo
ukiyabeza
Vyema kuhasa mtoto, hili pia lapendeza
Nimekuelewa sana, mama simpi lawama

Yeye
Asante kaka Masito, kwa tuliyozungumza
Kwa malezi ya watoto, ni kanuni
kuwajuza
Ili waukwepe moto, na maradhi kuuguza

Tuwasomesheni wana, tuwafunze yalo
mema

Mimi

Imekuwa changa moto, na mie nasisitiza
Tuwaleeni watoto, wazazi kamba kukaza
Jukumu hili ni mwito, sote wazazi
twaweza
Atwongoze Maulana, alo Mola ye Karima

Yeye

Iwe kulia kushoto, pembe zote
kuchunguza
Hii dunia mapito, na tena inapoteza
Tuwaombe watoto, njia njema kuongoza
Kwa uwezo wa rabana, tukakae pelo
wema

Mimi

Nahitimisha Masito, shairi tumemaliza
Tulosema si utoto, nanyi muone ni viza
Malezi mema watoto, tukiondowneni kiza
Twambizaneni kwa sana, heshima apewe
mama

MIIKO (SEHEMU YA KWANZA)

Babu

Mbona una wasiwasi, kipi wataka

kusema!?

Unayo ipi tetesi, nakuona umekwama!?

Kipi kinakusumbua!

Mimi

Babu naomba nafasi, nipate yako kalima

Waliyosema unasi, mambo yao toka zama

Naridhia kuyajua!

Babu

Sogeza kidago keti, wala usirudi nyuma

Kukujibu ni shariti, kwa mie mtu mzima

Kipi wataka kujua!?

Mimi

Acha nikaze sauti, nisiwe ninatetema

Tayari nimekeleti, nikiisaka ilima

Mengi nataka kujua!

Eti kupiga miluzi, usiku huwa si vyema!?
Majini huwa ya wazi, nambwa
yatakuandama!?
Hivi nini haswa huwa!?

Babu
Wakatisha usingizi, wengine wakikoroma
Ni kelele limaizi, ndo likaonywa mapema
Wenza usiwasumbua!

Mimi
Usile sufuriani, hunikanya wangu mama
Eti taozwa mvuani, harusi ikiandama!?
Hivi hili nalo huwa!?

Babu
Mja kula sahanini, hilo ni la tangu zama
Maadili usikhini, ndivyo akukanya mama
Wala si ndoa na mvua!

Mimi
Kujifunika uteo, eti kimo husimama!?
Ufupi ukawa cheo, au hii ni tuhuma!?

Ewe babu fafanua!

Babu

Hilo huwa pepeteo, wala lisikupe homa
Ulishike tangu leo, vyombovyo tumia
vyema!

Ni hilo babu tambua!

Mimi

Nnayo mengi maswali, ni mda
umeyoyoma

Twende kwanza tukaswali, hili kwetu ni
lazima

Machache nishachukua!

Babu

Usihofu ndugu Ali, nimeshaswali mapema
Hapa nasubiri wali, nipumzike mapema
Ruhusa hiyo chukua!

Mimi

Nikitoka mswalani, napitia kwa Alma
Hivi nikamwambieni, kwa haya
niliyosoma
Asijekunizuzua!

Babu
Mwambie akuamini, usiumie mtima
Mridhiane yakini, kama zama za Fatma
Awache kujishaua!

Mimi
Kwa heri babu kwa heri, na ubakie salama
Atujalie Qahari, kheri nyingi na neema
Hadi akituchukua!

MIIKO (SEHEMU YA PILI)

Babu

Huamki mjukuu, asubuhi ya Karima
Umelala mda huu, au ndwele mekuvama
Lakupiga meno jua!

Mimi

Ah! ni utosini juu, kichwa babu chaniuma
Japo kiasi nafuu, sana siwezi lalama
Na umenishtua!

Babu

Asubuhi umeswali, umepitiliwa ama!?
Na vipi yako maswali, unalo wataka
sema!?
Pole kwa kukushtua!

Mimi

Naam nimeiswali, jamaa nimesimama
Maswali nna mawili, kichwani
yamenandama
Nijuze lilo murua!

Usiku nikifagia, naambiwa sio vyema

Ni nuhusi najitia, mama hili kalisema
Hili babu walijua!?

Babu

Ni kiza kikiingia, taka utawacha nyuma
Hapatakati sikia, utakushangaa umma
Hilo nimelifumbua!

Mimi

Hapa hapa kwenye kiza, nimesikia
shutuma
Chumvi wakiniagiza, jina kutaja lawama
Na hili utafichua!?

Babu

Ni ungwana watimiza, kujiekea heshima
Wenza utawashangaza, mekuwa wapi
mapema!?
Chumvi si ya kupungua!

Kusema dawa ya mboga, lina nyingi
taadhima
Wajuwe utakulaga, kitoweyo nayo sima

Kwa hivi ushatambua!?

Mimi

Hayo nimeyanakili, walobuni wanadama
Ni kweli wana akili, na nyingi zao fahama
Hayo nimeshayajua!

Babu

Mimi nenda kwa Morowa, huko kuna
chetu chama
Nisije nikachelewa, wenzangu
wakanizoma
Acha nianze na dua!

Mimi

Wende ukibarikiwa, na mkajazwe neema
Na huyo maji ya mvuwa, mwambie nipo
salama
Mwambiye nimeshatua!

Namsubiri Zubeby, asema aja kusoma
Naja mfunza silabi, atunge zake nudhuma
Utunzi ataka jua!

Babu

Akija nisalimie, mwambie asinihama

Mimi mwenzangu ni yeye, mbona anitia
homa!?

Yeye ni yangu afua!

Mimi

Usinichekeshe mie, kwa hayo unayosema

Jitoto lenyewe ndie, babu hutoweza
ngoma

Ulimaliza kifua!

Babu

Nlijua utakerwa, haya ubaki salama

Mbeleni nisijeporwa, niambwe
nimeterema

Haya najitutumua

MIIKO (SEHEMU YA TATU)

Mimi

Eh babu sabalkheri, vipi hali yako njema!?
Kwa jaala ya Qahari, nimeamka salama
Haliyo nataka jua!

Babu

Naam sabaha nuri, namshukuru Karima
Wallahy afya nzuri, si vyema nikilalama
Natumai ushajua!

Mimi

N'sifia msafara, wa jana ya chenu chama
Nami nipate twasira, hwenda
nikawaandama
Au kinakusumbua!?

Babu

Sio kwamba wanikera, niungulike mtima
Chama kina nyingi sera, twataka anza
kulima
Kija msimu wa mvua!

Vipi jana mwanamwali, alikuja akasoma!?

Ama mliweka mbali, mkacheza baba
mama!?
Mana weye nakujua!

Mimi
Hahaha nacheka Ali, kwani hilo
lakuuma!?
Kuja huku mwanamwali, alifata ya
kusoma
Mengine wataka zua!

Hili babu unijibu, nisishike tena tama
Mana lanitia tabu, mama sana hulisema
Na bado sijang'amua!

Alo mimba kumruka, eti tumbo hukuuma
Maumivu humtoka, kwako yakakuandama
Na wewe ukaugua!?

Babu
Silielewi suala, kuruka unavyo sema
Iwe awe amelala, au awe yupo wima!?

Na kipi chakuugua!?

Mimi

Iwe awe amelala, usingizi akoroma
Maumivu mbadala, yake hukufwata
nyuma
Eti hivyo waugua!?

Babu

Eh! si hilo lipo wazi, ni kuepuka zahama
Na huo ni upuuzi, kumruka wima wima
Si kwamba utaugua

Waweza kumkanyaga, ukamtoa kinyama
Hasara ukapataga, asije zaa daima
Kumkwepa ndo afua!

Mimi

Hapo nimekuelewa, na kweli umeisema
Na hilo hawakuzuwa, walilijuwa mapema
Wahenga walitambua!

Sawa babu nakuacha, ya shuleni naifuma

Naona kumeshakucha, nazengea ya
kusoma
Zidi kunombea dua!

Babu
Kuomba siwezi acha, hiyo naitwaa dhima
Wala siwezi kuficha, nakuombea salama
Uzidi kujitambua!

UGONJWA

Namhimidi Manani, kwangu huu ni
wajibu
Utungo naweka chini, twaliini taratibu
Muyatie fikirani, mana hili ndilo jibu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Nisikizani makini, nayanena kwa adabu
Teja msimlaani, haimfai adhabu
Dawa tumnaswihini, tumuwekeni karibu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Ni ndugu zetu amini, tusioneni aibu
Katu tusiwatengeni, japo waleta dharubu
Kawatawala shetwani, Wallahi wapata
tabu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Kuwatia gerezani, sio siri twaharibu
Warudipo mitaani, huuzudisha uzibu
Tuwaleteni tibani, hili haswa ndo jawabu
Ni ungojwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Waje wafunzwe kanuni, huwenda wakaja
tubu

Watasahau zamani, wawe wastaarabu
Nasema tusiwalani, vizuri tulijaribu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Mfano u hai sini, mimi kuwa mraibu
Wema sikuuthamini, niliteswa aghalabu
Ila sasa nafuuni, kudunga sina sababu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Endapo hamuamini, haya niliyokutubu
Nifuateni nyumbani, mniulize khatibu
Tupo wengi kama nini, Sasa hatujisulubu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

Kalamu naweka chini, nishakifunga kitabu
Dua namwomba manani, aongoze waraibu
Waepuke mitihani, toba wawahi kutubu
Ni ugonjwa uraibu, mateja tuwatibuni!

MDUDE

Si kujuwa Mwalipembe, kuhasa ikilazimu
Si kwamba mie mpambe, panginge
munishutumu

Si hivyo muje nichambe, ninenalo si
wazimu

Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si mgovya wa maembe, hili lipeni elimu
Si mtamu siurambe, mdude huu ni sumu
Si mziki muuimbe, katu haujawa tamu
Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si ukoko uukombe, nisikiyani walimu
Si kilo wala si tembe, utakiweka pagumu
Si limbo ulimbe limbe, likanye hili imamu
Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si mchezo wa mdembe, m'pandishe mumu
humu

Si chombezo mlichombe, mdude ukupe
hamu

Si mzuri ni uzembe, shika la kwangu
gulamu

Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si butu huu ni wembe, jikate ujilaumu
Si m'vumbo uuvumbe, ukachukiza kaumu
Si kukimya nisigombe, munkari ukadumu
Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si mzizi uuchimbe, ikwaribikie jumu
Si hivyo uambwe kumbe, wabongo
wakwambe ndimu
Si ujanja usitambe, bure wajitia pumu
Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si shombe ni shombe shombe, udimuke
dimu dimu
Si famba uje lifambe, wenende ukinaumu
Si hayo usipayumbe, unatile kana gamu
Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

Si fumbo eti nifumbe, hapa mwisho
likitimu
Si uongo we kiumbe, usipoteze taimu
Si yangu na Mwadzilambe, zingatia
mwanadamu

Mdude hunu mdude, si mdude kujaribu

JANGA

Kwa isimu yake Mungu, nduza
nawasalimiya
Hamjambo ndugu zangu, hali zenu
najuliya
Nna ukumbusho wangu, kukumbusha
napaniya
Mihadharati ni janga, vijana
twaangamiya!!

Sitoyanena kizungu, useme hukusikiya
Tahadhari we mwenzangu, usije
ukapoteya
Uteja tele machungu, waja watakuchukiya
Mihadharati ni janga, Teja leo nakemeya!!

Hazitokutoka pingu, gereza utaingiya
Kila siku ni marungu, maisha yalo udhiya
Utakujaa ukungu, shida na madhila piya
Mihadharati ni janga, Wallahy utaumiya!

Zama za uteja wangu, mengi niliyapitiya
Nawahasa nyi wenzangu, uteja hiyo si
njiya
Hilo ni haramu fungu, motoni wende
ishiya
Mihadharati ni janga, limeisibu duniya!
Ilivyo tangu na tangu, kukanyana ndo
sawiya
Sitonyamaa mwayangu, ujumbe
kufikishiya
Lanitoka chozi langu, nikifikiri naliya
Mihadharati ni janga, jiepushe
nakwambiya!

Si wadigo si wazungu, si china si arabiya
Meathiri ulimwengu, kula rika wabugiya
Tanga Lamu Takaungu, hakuna palosaliya
Mihadharati ni janga, dunia yote yaliya!

Kilivyo tanda kiwingu, tumlilie Jaliya
Mwenye aridhi na mbingu, sahali
kutujaliya
I juu mikono yangu, nanyi dua itikiya

Mihadharati ni janga, Mola
atatwepushiya!

Tama ya shairi langu, nafusini naumiya
Teja kuwa jina langu, mengi
nayakumbukiya
Yasikufike mwenzangu, utajuta utaliya
Mihadharati ni janga, si janga la
kuchezeya!

NI MTU

Nakaa chini kutunga, nnazo nyingi hisia
La huyu mla maunga, asowacha kusingia
Tusimuone mjinga, kwa zizo zakwe
twabia
Teja na yeye ni mtu, naye yuna haki zake!

Ngawa mbii nyendo zake, si wa ila kumtia
Haifai umcheke, sui kummiminia
Tumwombee alivuke, janga alilojitia
Teja na yeye ni mtu, pia ana wake watu!

Japo hudhulumu watu, kukicha kuwaibia
Roho msitie kutu, moto kuwachoma pia
Tuwaonyesheni utu, hwenda wakaona njia
Teja na yeye ni mtu, inawafaa nasaha!

Nsemalo si mzaha, tuwache kuwachukia
Hivi wapataje raha, jela ukenda mtia
Wamzidisha jeraha, akitoka arudia
Teja na yeye ni mtu, ana haki ja wengine!

Na atibiwe apone, inusurike dunia
Tumjali ajione, isiwe twamkimbia

Na tusim'banebane, jangani akabakia
Teja na yeye ni mtu, tuwahurumie jama!

Kumnyanyapaa noma, Illahi hajaridhia
Tujuwe hakuna mwema, yeyote
aweangia
Tutwaeni hii dhima, iwe twamsaidia
Teja na yeye ni mtu, awavyo ni
mwanadamu!

Kaukosa utimamu, uteja kuuvamia
Ila la kumuheshimu, latupasa nisikia
Yani tusimdhulumu, akatulani Jalia
Teja na yeye ni mtu, ayapitiayo mengi!

Uteja kamwe si'ungi, sima mkanililia
Ila langu la msingi, tuwe tukiwausia
Mana nayajuwa mengi, uteja nilipitia
Teja na yeye ni mtu, yapaswa
kumuombea!

UTENZI WANGU

Kwa jina lake Karima
Mola Mlezi daima
Mungu wa zama na zama
Mimi namshukuriya

Kanijalia wasaa
Kitako chini nakaa
Kalamu ninaitwaa
Utenzi kuandikiya

Aniongoze Jalali
Nipate kile kitali
Tena kwayo njema hali
Mwisho nikipafikiya

Anisitiri ulimi
Zifike mia na kumi
Beti zilizojihami
Yombo zisijepitiya

Anijalie uwezo
Nisiandika muozo
Vithibitike vigezo

Hili liweze timiya

Ni themanini na moja
Novemba tarehe moja
Mamangu bila harija
Kanizaa nawambiya

Furaha tele bashasha
Famili kufurahisha
Haikuwa mshawasha
Ali kaona duniya

Mie ni mwana wa kwanza
Wa wazazi kujifunza
Kwa wema wakanitunza
Na mapenzi miya miya

Walinijali hakika
Kunipa ninachotaka
Nyoyo zikadigirika
Malezi nilokuliya

Wakanilea kwa kheri
Hawakuitaka shari
Walikuwa majasiri
Mema wakanifunziya

Nilianza chekechea
Siku zilivyosogea
Masomo kuyaendea
Ya akhera na duniya

Madirasa nikatiwa
Ya dini niweze pawa
Mengi niwe naelewa
Isinighuri duniya

Kukuwa nakuwa mwana
Shule nayo ikafana
Sikuona ikibana
Vizuri liendeleya

Nikawa mwana mwerevu
Mjanja na msikivu
Wala sikuwa mvivu
Masomo kazingatiya

Nikajiunga msingi
Shule ya Waa bodingi
Japo wanafunzi wengi
Namba nikashikiliya

Nilikuwa namba wani
Siku zayo mitihani
Zawadi kocho pomoni
Nyingi lijinyakuliya

Nikajaliwa talanta
Boli nikalisakata
Uchezaji wa matata
Wengi walinisifiya

Darasa hilo la saba
Boli langu marhaba
Haswa kiwa namba saba
Mabao niliyatiya

Siku moja mazoezi
Wanafunzi wazi wazi
Nikaona ya manyezi

Bangi wanajivutiya

Nambwa mambo iko huku
Ewe Teja njoo huku
Vuta bila ya shauku
Hao waliniambiya

Hapo nilivuta bangi
Nakujiona ni kingi
Likatembezwa na tungi
Pombe nikajinyweleya

Ikawa ni uraibu
Bila bangi yawa tabu
Mpira huwa dharubu
Niicheza naumiya

Nikawa bado nacheza
Ila masomo napuza
Walimu nikawakwaza
Kwa mbovu zangu tabiya

Tabia zikawa mbovu
Nidhamu mwana mtovu

Hadi nikanuka lovu
Na chuki ikaningiya

Mwaka tisini na tano
Kwa mengi mafarakano
Madhila pia miguno
Mtihani likaliya

La nane nikahitimu
Na wala sikulaumu
Kwa ninavyo kula ndumu
Sikufeli nawambiya

Hapo nikaitwa Kwale
Ya waume peke shule
Ya upili ndio ile
Kidato nikaanziya

Bangi ilinitawala
Nisingeweza kulala
Na pia sihamu kula
Bila ya kujivutiya

Shuleni na marafiki
Nikidhani ndiyo kiki
Ya walimu siyataki
Kumbe ninaangamiya

Cha pili nilipofika
Nikahisi kutoroka
Ilikuwa pata shika
Kusoma nikachukiya

Tukaupanga mgomo
Nikawa mbele kidomo
Bweni likachomwa chomo
Mgomo ukatimiya

Nikafukuzwa shuleni
Nikarudishwa nyumbani
Sitakiwi asilani
Walimu wajisinyiya

Ilikuwa ni bughuda
Maisha kishida shida
Nikawa sina faida
Nikaonwa ni m'baya

Nikenda hadi Likoni
Kwa bibi kwake jikoni
Na machozi ya shavuni
Naliya Ali naliya

Bibi alinituliza
Na mengi kaniuliza
Yote nilimueleza
Kaninyamaza kuliya

Mie nitakusomesha
Haya ni yako maisha
Nayo bidii onyesha
Yako yaweze timiya

Daru Ulum tukenda
Hii shule nikapenda
Maovu sikutayatenda
Nafusi ikatuliya

Siku moja michezoni
Nikamtia machoni
Nilompa namba wani

Fatuma limzimiya

Alivyoumbwa banati
Nilihisi ni bahati
Nikamuenzi mnati
Na kwake nikajifiya

Masomo huku mapenzi
Na yeye akanienzi
Na sote tu wanafunzi
Ila tukayaridhiya

Kwao kwetu walijuwa
Kwamba nitakuja owa
Nasi tulivyo chachawa
Tulionyesha duniya

Mapenzi nipe nikupe
Nipende mi ninenepe
Roho zikawa nyeupe
Mapenzi tukazamiya

Sikumbuki kosa gani
Sijui lifanya nini

Akanitenga mwandani
Yangu hataki sikiya

Sikuwacha kulalama
Uliniuma mtima
Nafusi akaichoma
Kanitosa mai diya

Tafrani na tewengu
Kunitosa huyu wangu
Machungu tele machungu
Katamani kujifiya

Banati nilompenda
Alinitia kidonda
Kweli nami nikakonda
Uchao kumuwaziya

Hapo kidato cha tatu
Roho ikajaa kutu
Sikusikiza ya watu
Uteja nikaanziya

Nikaingilia unga

Na bangi sikuitenga
Roho yangu kuiunga
Mawazo kupotezeya

Sikuzengea kusoma
Uteja ukanivama
Nikalivaa zahama
Nikaipotea njiya

Mwaka wa elifu mbili
Nikahitimu rijali
Elimu kaweka mbali
Kijiweni kaingiya

Uteja jama uteja
Nikazidisha uteja
Sikuweza ngoja ngoja
Watu nikawaibiya

Wengi niliwadhulumu
Hali ikawa ni ngumu
Hata ndugu zangu damu
Mabaya kawafanyiya

Niloyafanya ni mengi
Mambo yasiyo msingi
Eti kusaka shilingi
Shimoni kwenda itiya

Nikikumbuka naliya
Teja mie naumiya
Namliliia Jaliya
Msamaha natakiya

Katika siku za siku
Sioni wala sishuku
Uwizi ukanipiku
Wakanishika raiya

Za mwizi arobaini
Ningechomwa si utani
Nusura yake Manani
Polisi wakatokeya

Nikapelekwa polisi
Nakufunguliwa kesi
Mashitaka ya uasi
Kizimbani kafikiya

Nilijihisi ni mfu
Kesi ilokuwa rafu
Haikuwa unyoofu
Ikanikumba hatiya

Kesi wizi wa mabavu
Kunyang'anya kwa maguvu
Hapo ninyongwe laivu
Ikihakiki hatiya

Elifu mbili na tano
Kikanikumba kibano
Maamuzi ya mifano
Hukumu kanishukiya

Gerezani nikasota
Tamaa niliikata
Shingo yangu watakata
Siku ninayongojeya

Nilijua nimekwisha
Mwisho wa yangu maisha
Gereza linikondesha

Jela nilivyochukiya

Maisha ya gerezani
Kukumbuka sitamani
Tukawa ja hayawani
Udhiya tele udhiya

Nikalizowea jela
Kuyafumbata madhila
Nikaridhia usela
Hali nikakubaliya

Ikaja mwaka wa kura
Wachaguzi nazo sera
Mambo yao nyara nyara
Debeni wakazitiya

Elufu mbili na saba
Kibaki kashinda baba
Akaushika mkoba
Kiti kajinyakuliya

Kwa heshimaye raisi
Akatujali na sisi

Akatupa na nafasi
Tusinyongwe kawambiya

Kiwe kifungo maisha
Kunyongwa kabadilisha
Hukumu akashukisha
Wengine kaachiliya

Nikazurura majela
Kamiti pia melala
Naivasha nilikula
Manyani Malindi piya

Elifu mbili na nane
Wakataka wanione
Kotini twende tunene
Rufaa lijikatiya

Ya Mungu uwa ni mengi
Sijidai na siringi
Wakaamua madingi
Nikawa huru raiya

Teja nilifurahika
Mwili ukatetemeka
Nafusi ikapetuka
Raha nikajihisiya

Nikarudi mitaani
Mule mule utejani
Maisha ya vijiweni
Nikazidisha ubaya

Ubepari ufidhuli
Na kiburi imi nduli
Sikuyataka maswali
Uteja kaangaziya

Nikaja iba kwa mama
Nilivyokosa huruma
Wallahy moyo wauma
Allah tanisameheya

Mama alivyoudhika
Lipo alilo tamka
Teja nikatabwarika
Uwizi nikachukiya

Sikwamba likuwa chizi
Kwamba sikuwa na kazi
Ila yote matatizi
Machupa kajizoleya

Mburu mburu magunia
Majaani liingia
Masikirepu sikia
Nikawa natafutiya

Kuvuta ikawa ovyo
Kudunga kaona ndivyo
Uteja hivyo ulivyo
Sindano nikadungiya

Miaka kumi na tatu
Mepotea mwana watu
Hivyo kukutu kukutu
Miaka kipotezeya

Siku moja kijiweni
Wakaja kina fulani
Na mema yao maoni

Kutaka nisaidiya

Nami nikawa tayari
Nilivyokuwa na ari
Kiwa ni jambo la kheri
Yao nikayasikiya

Nilitiwa mjengoni
Nikawa matibabuni
Nami katika imani
Uteja nikaachiya

Hivi sasa nipo huru
Si uongo nashukuru
Sipanii mkufuru
Alonijalia haya

Naishi kwa yangu tosha
Nafurahiya maisha
Shukurani naregesha
Kwa walonisaidiya

Sitaki mi kuwataja
Walio nipa faraja
Nikabahatika mja
Leo nayaandikiya

Yalo bora ndio bora
Sikuona nawakera
Msamaha kitu bora
Wazazi liwatakiya

Baba nae wangu mama
Pamoja tumeungama
Nenda nao wima wima
Maisha nasherekeya

Nami sasa nishaowa
Vidume vikazaliwa
Yote haya majaliwa
Kanitunuku Jaliya

Ni bahati iliyoje
Mi mwenzenu nisemeje
Au nanyi mwaonaje
Haya niloyapitiya

Leo yangu majukumu
Niwezacho najikimu
Maisha bila sitimu
Wallahy nafurahiya

Ningalikuwa malenga
Mashairi ningetunga
Vina ningelivipanga
Isomwe historiya

Ningeandika kitabu
Hata kama kiarabu
Endapo watakhutubu
Waweze nikumbukiya

Ama niutunge wimbo
Waimbe bila mafumbo
Uje nienzi mkumbo
Nikiiaga duniya

Yalopita yalipita
Na mbele siwezi sita
Nilipo sasa nakita
Uteja sitorudiya

Ninaijali jamii
Kusaidiya sivii
Kamwe situlii jii
Daima nasaidiya

Janga hili mlijuwe
Maombi nawaombewe
Utejani tuwatowe
Wale waloangamiya

Hii yote ni safari
Jaala yake Qahari
Ni makini msafiri
Hapa nilipofikiya

Mikono nainyanyuwa
Naiomba yangu duwa
Nizidi kubarikiwa
Qudura naipokeya

Mnisamehe wangwana
Nilowakosea jana
Sinifanyie khiyana
Chini nawaangukiya

Iwapo nikufidiya
Ni tayari nawambiya
Wala sio kwa ubaya
Radhi ninazitakiya

Roho ziwe maridhawa
Sote sie tuwe sawa
Kwa kila alokosewa
Samahani nawambiya

Siandiki kwa fahari
Wala sio ujeuri
Yote ni kutaka kheri
Mola atanijaliya

Ingawa sina majibu
Uteja jama dharubu
Mtu asiujaribu
Atajitiya udhiya

Nitakao mwisho mwema
Aniruzuku Karima
Nimiminie neema
Kwako nikisujudiya

Naomba mnikubali
Nilikotoka ni mbali
Ninazo nyingi dalili
Wallahy niliumiya

Ameniwezesha Mungu
Akanipa langu fungu
Leo sioni majungu
Raha ninajionea

Japo nilifanya mengi
Nimekuwa kama kingi
Na wala imi siringi
Nambwe najiropokea

Nikivikumbuka visa
Ilonikuta mikasa
Teja wakati ni sasa
Kunawiri napaniya

Mia na kumi ndo hini
Kalamu naweka chini
Anwani nasaini
Mwisho nimepafikiya

SHARITI LAO WAZAZI

Mimi: Kuhaswa ninakutaka, nikwombapo samahani

Kila napo kukumbuka, nilokutenda zamani

Utejani nishatoka, mama kwako nipo chini

Radhi zako nazitaka, nisamehe kwa yakini

Mama: Leo nimefurahika, yamkini siamini

Mema unayotamka, kukuhasa natamani

Mamako nimeridhika, nahisi raha moyoni

Ni shariti kulishika, usirudi utejani

Mimi Nahisi ningapalika, nikirudi utejani

Shariti lako nashika, ni horomo kijiweni

Kwa hapa nilipofika, uteja uwe wa nini

Mama radhizo nataka, sharitilo likichwani

Mama: Iwe kheri na baraka, akhera na
duniani Akuhifadhi Rabuka, ende kutia
peponi

Leo mamako nacheka, fundo sina
mtimani

Shariti ukilishika, sikuachi asilani

Mimi: Kiapo nakitamka, sitorudi
maungani Damu yanisisimka, nakubusu
kipajini

Sasa baba namsaka, nae nimueke chini
Radhize pia nataka, nimtake samahani

Mama: Mwanangu tasalimika,
nakwombea kwa Rahmani
Kwa babako ukifika, sisaze ya fuadini
Zamani aliudhika, ila tia tumaini
Shariti langu kumbuka, usirudi utejani

Baba: Simama ulipofika, kwangu weye
watakani
Nini kwangu wakitaka, au mesahau nini
Nasema wewe ondoka, nisikuone
machoni

Bakora niloishika, itakwishia mwilini

Mimi: Si kwa ovu mi kufika, baba kwako
nawa chini

Najua uliudhika, kwayo mengi ya zamani
Ila kwako nimefika, kukuomba samahani
Radhi zako nazitaka, nisamehe ya zamani

Babu: Mungu Mkubwa hakika, kwa hili
sijaamini

Kheri uloitamka, subutu nikakukhini
Mwili wanitetemeka, ila menipa imani
Iwapo radhi wataka, nikutie sharitini

Mimi: Sharitilo talishika, siliwachi
abadani

Kwa uwezo wa Malika, baba jipe tumaini
Baba naomba ridhika, nami niwe furahani
Sema yatayosemeka, niridhie asilani

Baba: Iwe limebainika, kutorudi utejani
Vyema ushabadilika, usirudi kwa zamani
Radhi hadi kunizika, siporudi utejani
Shariti lishasikika, nakusamehe yakini

Mimi: Nami yako meyashika, nayaweka
sudurini

Upya leo mezalika, simi Teja wa zamani
Shariti nitawezeka, baba yangu niamini
Radhi zako kuzisaka, imetoka mtimani

Mimi: Wazazi mlosifika, nasema
ahsanteni

Shariti nimelishika, siliwachi si utani
Raha nimekubalika, nyuma nirudie nini
Radhi zenu kuzisaka, kanijalia Manani

SIRUDI KINANI

Namsabihi Ghafari, Mola wa viumbe
vyote

Mjuzi siri dhahiri, anayetujua sote
Leo la kwangu shairi, wajuwaji sinisute
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Sijaijuwa bahari, nahodha siteme mate
Na huu si ubepari, kama hori nilifate
Ngangari tena jasiri, hadi nizimbue chete
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Hainitishi shuwari, nanga nabwaga popote
Nikajichezea jori, nirudi kumwaya nyute
Ima nihisi bohari, chomboni nijiburute
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Sinipe shipa la ngiri, la kuvuta nikuvute
Ukanipandisha mori, unene mi si chochote
Safari tele mazuri, sendi nikabwiya kete

Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Dau litele johari, acha Mudiri nidate
Mawi yamekuwa kheri, kama keki niikate
Sio siri ya sufuri, waja munifatefate
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Sijifutui kidari, vidole kesho viote
Nambwe Teja nyiri nyiri, nao wanga
wasalate
Kisinfike kiburi, thawabu mie nipate
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Hakinipati kideri, eti domo linibete
Naitambua sayari, na vilivyo humo vyote
Zishanisinya ndodori, duvi ndio nitafute
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

Tamati jama kwaheri, nawaaga nyie nyote
Kwa upole na uzuri, nasema musinifate

Hiki kina cha bahari, kwa guu sikitafute
Ya pondo mefunga tanga, wala sirudi
kinani

VISAWE 1

Tasa mfanowe tatu, isoganyika kwa mbili
Tasa ni hazai katu, kwa jaala ya Jalali
Tasa ni chombo cha watu, hunawia ja
bakuli!

Tembo huleweshwa watu, zikawaruka akili
Tembo samaki si chatu, huwa manjano ki
mwili
Tembo haachi msitu, makaziye ya awali!

Kiwi ni roho ya kutu, haikufai rijali
Kiwi si silaha butu, ya ngisi ienge mbali
Kiwi ndege mtukutu, ja kitwitwi yake hali

Kina cha hapa ni 'tu', silabi mwisho kamili
Kina soma mwana kwetu, usomi usidhalili
Kina kirefu si kitu, shimo hatutobadili!

Angua sio upatu, lia twakona jahili
Angua matunda mwitu, yatawafaa ahali
Angua yai lako tu, kuku sikwambi fahali

Koma mwisho hapa shutu, mbele sisongei
Ali
Koma huvitenga vitu, alama ya kunakili
Koma huwa tunda mwitu, mpwani yupi
halili

VISAWA 2

Hapa naanza si tama, udhani ipo mwishoni
Wala usishike tama, mkono toa shavuni
Hayo maji pata tama, usome kwa burudani

Ebu chini weye kaa, usikize nasemani
Usiwake kama kaa, utanichoma mwendani
Simi mlaji wa kaa, aishiye baharini!

Vina mizani we panga, kuwa sawa lainini
Sio kukata na panga, silaha hiyo jamani
Usiichezee panga, wachawi wamumo
ndani!

Nyota yangu ina jaa, bahatiyo si utani
Mazuri kwangu yajaa, yanafurika pomoni
Simi wa kwendea jaa, huko uwa uchafuni!

Roho yangu isi tanga, natakwa niwe
makini
Au nilifunge tanga, nisafiri mashuani
Niende pwani ya Tanga, kulo wajuzi wa
fani!

Huko ntakula kamba, wavuliwao kokoni
Mashazi ufungwa kamba, mnyaa au katani
Si upishi wa Kikamba, kabila humu
nchini!

Uwa wazi langu fumba, mkono uimarani
Nakesha na sitofumba, jicho la usingizini
Sikwamba hini nafumba, si fumbo
mniamini!

Juwa mimi siye rudi, nyote
nawaheshimuni
Nenda mbele nyuma rudi, mwisho nipo
ukingoni
Ninapokosa nirudi, ili nijitathmini!!

DAFINA YA USHAIRI

Kwamba u gwiji wa tungo, jukumu lako
kufunza

Kamilisha lako lengo, ujue na pa kuanza
Utungapo kwa mpango, aina zinazo tanza
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kigezo kiwa kipande, kwa mistari kimoja
Ni utenzi usikonde, vina na urari taja
Tungo za kale na punde, maudhui ni
mamoja
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Mathinawi ni bahari, vipande vyake viwili
Ukwapi ukidhihiri, utao ndicho cha pili
Mizani kwa kikadiri, muwala siwe zohali
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kiwa vipande vitatu, bahari mbili baini
Na vina viwe vitatu, kwa idadi ya mizani
Zisizidi nane katu, ukawafi ndio shani
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Tumbuizo ni nyengine, vitatu vipande
vyake
Kipande mizani nane, mtajo silabi zake
Japo vina vipingane, mghani usisumbuke
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Bahari ya bantundi, vyake vipande vinne
Mtunzi awe ni fundi, mawazo
yashikamane
Kujipatia ushindi, kanuni zitangamane
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kikai kieleweni, mizani zabadilika
Ukwapi haulingani, na utao kadhalika
Kwengine mizani chini, zengine
zaongezeka
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Msuko wake muundo, idadi ya mishororo
Matamshi kwa mtindo, mmoja una kasoro
Kwa ufundi wa mtando, beti huunda
mchoro
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Neno unapokariri, mishororo kwenye beti
Msisitizo dhahiri, maudhui kudhibiti
Kikwamba ndio bahari, liwe mwanzo au
kati
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Pindu yataka stadi, kumaliza na kuanza
Kipande kukiradidi, cha mwisho kiwe cha
kwanza
Mtunzi awe shadidi, lugha isije mponza
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Na bahari ya ukara, ni shairi tofauti
Kina huwa chadorora, kwenye vipande
vya beti
Ila kimoja hurara, cha mwisho au cha kati
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Uwapo ukaraguni, usishikwe na tewengu
Kwa vina havifanani, kila beti lakwe
fungu
Na muundo asilani, si wa tungo za
kizungu
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kunao mtiririko, kwa mlingano wa vina
Zingakia ya beti zako, vina vyote
hufanana

Napo pawe makiniko, utunzi uweze fana
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kuna mseto wa tungo, wa aina na bahari
Pamoja kwa ufinyango, likawa moja shairi
Kilikamilisha lengo, sakarani ndo bahari
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Kuna bahari ya wia, pasi mizani na vina
Ni wimbo wajiimbia, hoja kuu ni maana
Tamathali kutumia, jazanda hufaa sana
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

Tama ewe mshairi, tuwa uikuze fani
Tungo zako zishamiri, ziwe zaleta maani
Situnge zilizo shari, za kukufuru Manani
Dafina ya ushairi, ni aina na bahari

FUNGA NYAMA

Malenga kila mahali, wabara na walo
pwani
Na walo nchi za mbali, za karibu na jirani
Nawaomba tafadhali, mada hino changiani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Mada hino maadili, kilumbano malumbani
Naweta walo kamili, zilo watuwa
vichwani
Timamu walo akili, wasije masakarani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Mahiri ngoi wa nguli, wa sasa na wa
zamani
Rahimu na mafidhuli, walo jadi za matani
Tuchezezane kauli, pasi na matusi ndani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Kijomba cha uswahili, kimvita chalo fani
Kimrima cha adili, kingozi kutamkani

Njooni tukijadili, kilahaja lahajani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Hariri tuzi halili, semi nyeti kuzibuni
Tafusida za asili, jadi lugha tamaduni
Asiliya tamuthili, nyia ziongowe nuni
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Kebehi na kukejeli, magowano kimatani
Mabezo yaso ya feli, pasi chuki na undani
Tuimbane kwa yaleli, pambalimba
uwanjani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Manju kibili mithili, watungi wao tungoni
Wasije kunikabili, mwanzoni hata
mwishoni
Wao hawasitahili, kuwamo mdahaloni
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Wa mama walo usuli, watunzi wa
majikoni
Wakufunzi wa sukuli, na vitoto vya
chuoni
Kando nawatuwe tuli, sibwabwaje
midomoni
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Watunzi bilali fuli, makanyo nawakanyeni
Wafyonzi mabaradhuli, ma dhudhu
mkanyageni
Wasijitie shughuli, kunidakiza uneni
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

Teja tama wafadhili, wamuzi wa barazani
Pimani hili kwa hili, kuishinde ushindani
Mshindi wa tandawili, tuzo na tuzwe
nishani
Kilumbano malumbani, funga nyama
ushairi

UGWIJI

Leo ni yenu malenga, majagina na
magwiji
Mlo bobeza kutunga, waimbaji waghaniji
Wa Mzizima na Tanga, Mombasa pia
Rufiji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Panga vina kuvipanga, onyesha wako
umbuji
Andika za kutuganga, waama zitufariji
Zisiwe za kusimanga, za kufana twahitaji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Tungani kuzifinyanga, eneza muenezaji
Ziwe na tele muanga, watu wasije zihoji
Za matusi kuzienga, ndio habari ya jiji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Fani msiiboronga, mchambane
wachambaji
Michambo usibananga, kutukana huwi
gwiji

Mafumbo unayofunga, lekeza
mwelekezaji!
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Sije cherana mapanga, damu damu
umwagaji
Madhila yakatuzonga, kujifanya wajuwaji
Wengine wakajitenga, ikose wadumishaji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Maungano kuyaunga, amani utengezaji
Wa biladi na viunga, upendo twauhitaji
Heshima iwe ni kinga, tusiwe wachafuaji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

Tamati nabwaga nanga, namaliza mtungaji
Poleni enyi malenga, labuda ni mkosaji
Niutakao ni mwanga, mawi tuwe
wakingaji
Tusionyane ugwiji, tujiepushe majanga!

UTAJUTA LIKITOKA

Neema zakwe Qahari, namuhimidi hakika
Kunga hini ishamiri, iwafunde kadhalika
Usomapo sighairi, kikosi chako inika
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Thamini Sana um'ri, fanza yano kubalika
Kakutunuku Jabari, ewe mja wajibika
Ulifatapo kaburi, usende kulalamika
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Unayo afiya nzuri, ndwele hazijakufika
Usiendekeze Shari, mwisho ukababaika
Utakuja tahayari, yamekuzidi mashaka
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Malizo eeh tajiri, zizengee kwa haraka
Zisikutie kiburi, zitakase toa zaka
Waja kosa ufahari, pindi zikikutoroka
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Ndoa isikughururi, uharakishe talaka
Suluhu huleta kheri, domo lisije kumaka
Utaliam sio Siri, hataki alokutaka

Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Jitanibu na hatari, silaha isiponyoka
Ima iwe mwenye gari, usukani vyema
shika

Walau wavira hori, Kasia isianguka
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

Tama kwako mshairi, yalo natija andika
Wino ukishadhihiri, na ujumbe utafika
Itunze fani hariri, ewe dada ewe Kaka
Utajuta likitoka, lote kwako lilo zuri!

OZWENI

Bisimika, ewe Qahari, tunza naanzia
Kwa hakika, hini ni kheri, nawakumbushia
Kusomeka, ni yangu ari, nawawaidhia
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Ushakua, ushabalehe, pata utulivu
Ni murua, kustarehe, kuwa msikivu
Ungajua, uliza shehe, ndoa si tukivu
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Uwa ndoa, nusu ya dini, jambo la thawabu
Uwe poa, sio uhuni, maisha ya tabu
Silo doa, usijikhini, sikia swahibu
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Utajiri, hupatikana, moyo ukinai
Sio siri, ndugu kijana, oa ujidai
Si ya shari, ya msichana, ndoa kuidai
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Ni jukumu, tukanyaneni, komesha uzinzi
Ni muhimu, tuwe makini, lisitupe ganzi

Na dawamu, walo ndoani, hao ndo
wapenzi
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Yangu hoja, ni ubachela, muupige teke
Si bwabwaja, na si kabwela, ozwa
mwana kike
Ipo haja, ndoa aula, ndizo tuzishike
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

Ni tamati, mnisikie, waume oweni
Yalaiti, siwafikie, demu wangojani
Ati ati, usingojee, haraka ozweni
Muungwana, oa olewa, upate sitara!

MAVAZI

WOTE

Tunamshukuru Mungu, Mola wa viumbe
vyote

Mwenye aridhi na mbingu, aloumba watu
wote

Hili la tangu na tangu, na sijataka tutete
Nayasema ya mavazi, vijana wanavyovaa!

MVULANA

Haswa nyie mabanati, Wallahy
mwatuzuzua...

Hivyo vi mini sketi, si siri vya waumbua!

MSICHANA

Ohoo mtenashati, kwa kipi
watutuumbua!?

Mbona unavaa shati, na kiko nje kifua!?

MVULANA

Hii yangu ndio swaga, si vinguo vya
kubana

Maungo twayaonaga, ebu badilika bhana!!

MSICHANA

Hahaha eti ni swaga, makalio kuyaona!?
Duza mnavyoibwaga, haijawa kwenye
Sunnah!

MVULANA

Ya sunnah wala faradhi, kamwe nyie
hamjui
Nguo zenu zinaudhi, bora liwe bui bui!

MSICHANA

Yapaswa uombe radhi, usemavyo hatujui
Mikufu inakukidhi, mume gani hujijui!?

MVULANA

Mikufu ndio fasheni, haya mambo ya
kisasa
Navaa hata hereni, zilivyo nijaa pesa!

MSICHANA

Rasuli alilaani, hebu zingatia sasa
Utajikuta motoni, huko hakuna cha pesa!

MVULANA

Kweli umeniambia, naanza kubadilika
Za nidhamu tavalia, nipate kuheshimika!

MSICHANA

Hata mimi nami pia, ulosema nitashika
Vimini sitavalia, za kubana kadhalika!

WOTE

Huu wetu ni wasia, tuvaeni za heshima
Maafa tusichangia, tukamuudhi Karima
Tufateni njema njia, ende kutuweka pema
Tuvae kujistiri, wanawake wanaume!

LIPUZE

Kwa uwezo wa mwenyezi, niatani
niweleze
Kulinyamaa si'ezi, kwa vivi nilifikize
Nalinena kwa uwazi, nanyi nyute msikize
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!

Usiwe wa domo wazi, na sauti upaize
Na wingi wa pingamizi, mpuzi kaka
mpaze

Tata yakwe utatizi, ndivyo nami nikubaze
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!!

Yachunguze maelezi, tafakari uyameze
Ikiwa hunayo kazi, vyemavyo yabebetuze
Yasikutia henezi, usona faidaze
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!!

Lakung'aza haling'azi, si kaziyo uling'aze
Wa kiza cha mbalamwezi, mwanga hajui
rahaze
Usijetumbuwa ozi, maonoye yapuuze
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!!

Mitezoyo hawatezi, na ya kwao usiteze
La upuzi hugeuzi, la maani sigeuze
Tena kwa nyakati hizi, upuzi sikupumbaze
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!!

Yawavyo ukimaizi, siongeze sipunguze
Kaa kando ubarizi, sio neno uengeze
Mpuze alo mpuzi, upuziwe sipatize
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!!

Kutunga kwangu ni kazi, atani niimeleze
Liepuke gozi gozi, pakupaweza paweze
Funguwani masikizi, upuzi siwatatize
Yamkini silikuze, lolote lilo upuzi!

UMECHELEWA

Hino yangu inyooshwe, iwe swala ya
Rahimu
Na wala isirefushwe, ikawachosha walimu
Si tungo wasikitishwe, maamuma na
imamu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Kwayo tungo ukumbushwe, sikasirike
imamu
Kwa hili usitingishwe, ukaikosa nidhamu
Si kiburi ukumbushwe, japo unayo elimu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Na pia usinunishwe, hujapokonywa
hatamu
Kuchelewa usitishwe, ukajitia ugumu
Yalo sawa uonyeshwe, uzingatie taimu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Usitake uteteshwe, useme twavuta ndumu
Hatutaki upwekeshwe, kama ulo na
wazimu
We subiri uswalishwe, ndo badae ulaumu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Swiratini urejeshwe, na wala usishutumu
Na sio moto uwashwe, ukajiona chokomu
Kwa ubaya usipashwe, lazima swala i
timu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Munkari upoweshwe, siambe sababu jumu
Kwa hili usidatishwe, bure upandishe
pumu
Tena usikasirishwe, ya vivi mambo ya
humu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwe!

Tungo hino isitishwe, mana swala
ishakimu
Ilivyo ni aswalishwe, angawa ye ni imamu
Maamuma usitishwe, ndivyo ilivyo kaumu
Umechelewa imamu, yalazimu
uswalishwa!

HALIKOSI

Wambuji sabalkheri, salamu ni zetu sisi
Nilipo natafakuri, ngawa nna wasi wasi
Nilitungavyo shairi, yanisokota nafusi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Hutupimia Qahari, imani zetu unasi
Yafaa tujihadhari, tumlani ibilisi
Isituzonge hatari, Rabbana tukamuasi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Nenda katowe mahari, ujipangie harusi
Watakuja wenye mori, watake tia nuhusi
Ima waje wanawari, wakikurushia nyusi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Fanya kaziyo vizuri, bighairi ya tetesi
Watazuka na viburi, wambe mehonga
nafasi
Wataka ulighairi, kwa vichocheo kwa bosi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Chonga kasia na hori, wende ukavue ngisi
Walio mbaya dhamiri, hawakupi ufanisi

Watachafuwa bahari, hadi huseme ni basi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Si siri ndege abiri, wende kusaka fulusi
Wataziponda dinari, fesibuku kwa matusi
Usipokuwa ngangari, utarudi ule bisi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Nawajuza washairi, ashakum si matusi
Komaa na mistari, si vitungo mwendo
Kasi
Isikuchome suduri, waambapo huwagusi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

Teja naamba akheri, dua pokea Qudusi
Rabba utupapo zuri, tufanyie na wepesi
Kula ajaye na shari, tukinge asitughasi
Mtihani halikosi, kula lililo na kheri!

IJUMAA

Siku hini Ijumaa, kaitukuza Wahida
Ndaniye ni manufaa, na nyingi nyingi
faida
Pia limumo jisaa, dua kujibu ni ada

Siku hini Ijumaa, jitayarishe mapema
Tena ujipe wasaa, umsabihi Karima
Kukwima au kukaa, uyatende yalo mema

Siku hini Ijumaa, swala ikiadhiniwa
Haraka usishangaa, kheri yakutanguliwa
Mapambo iwe kung'aa, manukato udi
sawa

Siku hini Ijumaa, isome sura Kahaf
Si siku ya kuzubaa, na kukithiri uchafu
Mswalani gaagaa, kwa hali ilo nadhifu

Siku hini Ijumaa, zipate hotuba mbili
Upuzi pia kataa, uzeng'ee ya Jalili
Maghfira yanafaa, mja usiwe jahili

Siku hini Ijumaa, swala ikimalizika

Hatua zako we twaa, fadhila kwenda
zisaka
Si vurugu ja mang'aa, anakuona Rabuka

Siku hini Ijumaa, dua ziombe kwa wingi
Usiwe kushaashaa, fanza yalo na msingi
Thawabu kapu kujaa, hufuta madhambi
mengi

Siku hini Ijumaa, tungo naiweka chini
Tutafuteni shufaa, tuzijengeni imani
Peponi nasi angaa, Mola akatutieni!!

NIZIKE NINGALI HAI

Umenitanda huzuni, njaa imekua kali
Dunia siitamani, kunizika afadhali
Nuru katu siioni, sina majibu ya swali
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Simkufuru Manani, likanikuta zuwali
Njaa hii hadi lini, maisha kama subili
Heri nikalale chini, nitangulize awali
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Nchi ikawa vitani, Teja hawakunijali
Wazazi wangu shimoni, waliwauwa rijali
Nimebaki matesoni, walobaki mabakhili
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Nitulize aridhini, nikaipoze akili
Dunia kichinjioni, imezatiti jedwali
Wao kutwa wa mbioni, kuhakikisha mi sili
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Msidhani hayawani, au nimekua nduli
Imezimwa darubini, sioni ya kunakili
Yanichoma fuadini, hali hii sio hali

Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Chozi tiriri shavuni, wanitetemeka mwili
Njaa hii njaa gani, menishinda kuhimili
Niwe hai nile nini, hiyo kwangu si halali
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Madhila yote pomoni, nimemkosa dalali
Uzunguni arabuni, kote nimekosa dili
Kifudifudi jamani, au unizike chali
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Malenga mutasemani, maisha yangu ya
ghali
Sisemi nipo sokoni, eti munionge wali
Mechokeshwa duniani, imenizorota hali
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

Tamati kalamu chini, dua namwomba
jalali
Tukirimu masikini, japo kwa ndogo dalili
Napiga magoti chini, medhofu kiwiliwili
Nizike ningali hai, dada njaa siiwezi

SUBIRA

Ewe Mungu, Mola muumba, uliesifika
Mwenye mbingu, ulieumba, pia malaika
Langu fungu, na sitoimba, Teja
naandika
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri!!

Wamba dhiki, zimesheheni,
usisononeka
Uzandiki, tele huzuni, ukasikitika
Babaiki, iwe la nini, na waweza vuka
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Ya dunia, huwa ni mengi, yatakuzunguka
Asilia, jambo msingi, hadhi kutovuka
Ukilia, uwa kigingi, mema yataruka
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Afadhali, kunyamazia, mawi kuropoka
Zote hili, kukubalia, wema utafika
Na maswali, yaso na njia, huko
kupotoka
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Hivyo hivyo, ujizatiti, imani kuweka
Mambo ovyo, piga kunuti, shida
utavuka
Na yalivyo, si ati ati, ukaghadhabika
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Yaillahi, muombe Mola, yatakunyooka
Sitizahi, iwe haula, usiborongeka
Usahihi, si zilizala, shida zitatoka
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Mja omba, iwavyo kinga, utasalimika
Si kutamba, yalokuzonga, ukaaibika
Kaza kamba, ulipo panga, yatakamilika
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

Ni tamati, yafika mwisho, niliyoandika
Khairati, ni ukumbusho, hutofadhaika
Jidhibiti, leo na kesho, utasitirika
Pa subira, mja subiri, mbele iwe kheri

NDIVYO ILIVYO

Nashika kalamu, ndivyo ilivyo, naandika
Utungo adhimu, ndivyo ilivyo, umefika
Na kwake Rahimu, ndivyo ilivyo,
naanguka
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Wala sitafumba, ndivyo ilivyo, eleweni
Si mchezo samba, ndivyo ilivyo, kwenye
fani
Msi kujigamba, ndivyo ilivyo, nathamini
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Ya hii dunia, ndivyo ilivyo, tunapita
Sijipe udhia, ndivyo ilivyo, wacha tata
Mwamini Rabia, ndivyo ilivyo, utapata
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Wapende wenzako, ndivyo ilivyo, ni sitara
Mja peke yako, ndivyo ilivyo, hutong'ara
Vichunge vya kwako, ndivyo ilivyo, si
hasara
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Amani amani, ndivyo ilivyo, itangaze
Kungia vitani, ndivyo ilivyo, siumize
Subira amini, ndivyo ilivyo, ieneze
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Iwapo jaala, ndivyo ilivyo, kushukuru
Sipende madhila, ndivyo ilivyo, ukufuru
Simamisha sala, ndivyo ilivyo, kuwa huru
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Zizi hizi pesa, ndivyo ilivyo, ni
shetani
Iwapo wakosa, ndivyo ilivyo, siwe duni
Na wakikunyasa, ndivyo ilivyo, jiamini
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Swala la mapenzi, ndivyo ilivyo, uwa zito
Mwenza kukuenzi, ndivyo ilivyo, sambe
ndoto
Palipo ushenzi, ndivyo ilivyo, kaza mato
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Ishu na maunga, ndivyo ilivyo, ufukara
Uteja kuunga, ndivyo ilivyo, taparara
Mambo taboronga, ndivyo ilivyo, si sihara
Ilivyo ilivyo, ndivyo ilivyo, hivyo hivyo

Zimekoma kumi, ndivyo ilivyo, ni tamati
Siwezi mangumi, ndivyo ilivyo, na
nanyuti
Nimo na sivumi, ndivyo ilivyo, sina cheti
Ilivyo ilivyo, ndivyo hivyo, hivyo hivyo

MFILIWA

Tumuhimidini yeye, Mola wetu msifiwa
Nakutubu msikiye, kanywani nnayatowa
Aambwaye kuwa siye, na yiye iye ndo
huwa
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Ja mti aukataye, ajabu kuangukiwa
Na rojo akorogaye, kujinywiliya ndo sawa
Hukaza afukuzaye, mbioze kutopunguwa
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Wachange wajichangiye, michango ya
kujaziwa
Mapishi wajipikiye, mapakuzi kupakuwa
Domoni asilitiye, hata pande la haluwa?
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Kibaba ajijaziye, na vitupa vya maziwa
Mwinyiwe afurahiye, ndogo ndogo
kuongowa
Yawaje ajinyimiye, ila hana la kupawa!?
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Nilengayo ni ndiroye, anavyo lilia dowa
Hawamaki mazaniye, vyake wavizowa
zowa
Zamchosha maye maye, kwani kipi
msojuwa!?
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Ni hini iwafikiye, mlio chini ya juwa
Yawavyo mtuambiye, kwa lipi
mnachachawa!?
Yaani afiliwaye, vilo vyake mwadokowa!?
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

Tama hapa niishiye, langu jina mwalijuwa
Ni mimi mwengine siye, Waa nilikozaliwa
Menipasa nitungiye, manake lanizuzuwa
Ni vivyo ya mfiliwa, aliwaye ndiye yeye!

DUNIA

Salamu nikianzia, mja itikia
Ndugu leo nakwambia, nawe nisikia
Napania kuusia, we sikilizia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Na sote tuwenda zake, tutajajifia
Ni vyema umakinike, ukifikiria
Ni nini kusudi lake, alo tuumbia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Tudumuni na ibada, na tukitubia
Kufanya mema ziada, hiyo ndio njia
Tutaipata faida, kifo kufikia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Tuyaepuke maasi, tutaangamia
Madhambi ni nuhusi, tutaja kulia
Simfate ibilisi, akafurahia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Siwaudhi walimwengu, watakuridhia
Sio mibaya mizungu, kuiigizia
Fanya apendayo Mungu, akikujalia

Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Usiwabeze wazazi, utajajutia
Kumbuka yao malezi, unajivunia
Kuwalea siwe kazi, hawataumia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Uwachane na ulevi, hiyo sio njia
Heri ukawa mvuvi, pato tapatia
Zitapokujaa mvi, usije jutia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

Mwisho nalihitimisha, kuliandikia
Ujumbe umeshatosha, umewafikia
Mengi nawe nikumbusha, nitakusikia
Hunenwa tambara bovu, ni hii dunia

HAYO HAYO

Leo sikifanyi choyo, niwaumize mioyo
Niazimani sikiyo, na musione tishiyo
Munambie kama ndiyo, na kama siyo si
hiyo
Nyi wenzangu mna hayo, au mna hayo
hayo!?

Keshawafikiya huyo, mja wa tele papiyo!?
Mtaani mbiyo mbiyo, afagiya kifagiyo
Yakwe ni hatari hiyo, kafwata za nani
nyayo!?
Hivi nyie mna hayo, au mna hayo hayo!?

Hatuji jayo tujiyo, kashikia shikiliyo
Aambwavyo yeye ndiyo, akiipapia miyo
Simfanze tegemeyo, apotoshe maishayo
Hivyo ya kwenu ni hayo, au mna hayo
hayo

Hujijia kwa pambiyo, akavutiya machoyo
Ajidai rafikiyo, akuwachie dhambiyo
Uadui mambo ja ‘yo, upotezwe
mwelekeyo

Kwani ko kwenu ni hayo, au mna hayo hayo!?

Laanaye marudiyo, kalanika na Molayo
Kujitia hamnayo, apambe muyafanyayo
Mukikoseka kwa hayo, ujitenga mbali huyo
Nauliza mna hayo, au mna hayo hayo!?

Utezeya imaniyo, mapotevu mapoteyo
Akaliye ndiya hiyo, uje upotee kwayo
Aifanzapo rahayo, akwezekeya kiliyo
Nijuzani kiwa hayo, au mna hayo hayo

Sabaa mwisho fikiyo, ichungile kauliyo
Yatoka ndani ya moyo, sio kuupiga mwayo
Jikanyieni na huyo, sende liya mayo!
Mayo!
Imi sijui ni hayo, au mna hayo hayo

NIROGE

Sisubutu niandike, kwa hubalo mwafulani
Mshiko wako nishike, unifiche maziwani
Nifanye nisizunguke, nitulie nawe hani
Roga dali nirogeke, nisahau wa zamani!

Nipa lote nitosheke, moyo pia na maini
Yamkini niridhike, yule nisimtamani
Niguse niweweseke, raha hadi mapafuni
Roga dia nirogeke, nisahau wa zamani!

Sitara nisitirike, bebi wangu niauni
Wajibu uwajibike, chumbani na kitandani
Nilishe nisitapike, uvipikavyo jikoni
Roga hani nirogeke, nisahau wa zamani!

Kanga kaza ikazike, itulie kiunoni
Nakupenda weye peke, tulizo la yangu
mboni
Vua vaa usichoke, vimini nazo bikini
Roga switi nirogeke, nisahau wa zamani!

Nitekerenye nicheke, kicheko cha ulaini
Kama chozi linitoke, kinitia furahani
Unidekeze nideke, nisiwe wa tafurani
Roga nana nirogeke, nisahau wa zamani!

Nichizishe nichizike, unigande akilini
Miropoko niropoke, kinipa vyako vya
ndani
Yowe langu lisikike, kiniweka kileleni
Roga mami nirogeke, nisahau wa zamani!

Canani pia nivuke, nivushe ewe ayuni
Niroge mwana wa kike, nyongo mkalia ini
Mambo yawe mwake mwake, nife nawe
ubavuni
Roga lavu nirogeke, nisahau wa zamani!

Tama naitamatike, bebi wangu njoo ndani
Njoo nijushikeshike, toka juu hadi chini
Nywele zitusisimke, tupelekane angani
Roga nirogeke, nisahau wa zamani

MIMI NAVE

Naandika, kwa uvezo vake M'ngu
La hakika, mana ndivyo kilimwengu
Nshafika, kwa nyondazo ve mwinzangu
Mimi nave, yasitukumbe matungu!

Nakupendra, vat'a n'kivunde t'ungu
Eve nyondra, tulidho la mboni dhangu
Hutokondra, umumo moyoni mwangu
Mimi nave, tule pendhi la kidhungu!

Sikuvati, ndilo tamko la kwangu
Ni bahati, tena ya tangu na tangu
Tafauti, sileti nikava bangu
Mimi nave, tudumu na dhetu pingu!

Nasimama, kukulaki nke vangu
Si lalama, kukupa vilivo vyangu
Na heshima, kwako ya tandra ja vingu
Mimi nave, changu chako chako changu!

Sikukani, moyo niupe tewengu
Walakini, haina nafasi pangu
Tathmini, nakupendra mwenza vangu

Mimi nave, hatutiani upungu!

N'naapa, tena kwa haki ya M'ngu
N'takupa, pendhi lote lilo kwangu
Kukutupa, sipanii mlimwengu
Mimi nave, hili ndilo letu fungu!

Hapa mwisho, sabaa ndro beti dhangu
Hata kesho, n'takuenzi kivyangu
Si vitisho, sivatishi valimwengu
Mimi nave, mimi vako veve vangu!

KUPENDWA RAHA

Mahaba nigaragaze, unifikishe Ukunda
Na uje unichombeze, kuthamini langu
tunda

Kwa uzuri ueneze, raha kupendwa
kupenda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba nipozepoze, moyo wangu
usikonda
Ima nim'bembeleze, kwa dhati navyo
mpenda
Subutu nimuumize, kwa huba lililopinda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba nigandamize, tena sinimwae
denda
Kwake penzi nitimize, haramu nikilivunda
Tucheze nae tucheze, si ja gemu la
kandanda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba nipatilize, metua kwake kamanda
Sipunguze niongeze, vyema nikaze
mkanda
Kwa madaha nibambize, na daima
takulinda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba nikazekaze, hata kiza kikitanda
Na mwenzu nisimlize, ajue ni chema
chanda
Penzi lisitukereze, hadi tuvishwapo sanda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba siniburuze, nonekane mie kinda
Na raha ifululize, nidandapo atadanda
Kwa manjonjo tufwatize, tusipeane
vidonda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba ninyang'anyize, msi pepo wa
marinda
Katu sinibebetuze, mapenzini nikavunda

Mapenzi yaso chochoze, sije nkameza
vwanda
Simuati wangu nyonda!!

Mahaba niimalize, hadhi yangu nailinda
Na maswali muulize, yupi anae nipenda
Tungo isiwatatize, yupo nnae mpenda
Simuati wangu nyonda!!

KISEBUSEBU

Kwa dharubu, lele inyamaze ngoma
Ni aibu, japo nataka kusema
Aghlabu, utungo mutausoma
mi n'na kisebusebu

Siwi bubu, ijapo nishaterema
Na majibu, moyoni yakanichoma
Masharubu, bado yananitetema
Mi n'na kisebusebu

Nawa zibu, sichoki kumchegema
Kubu kubu, uchao kumuandama
Taratibu, heri nirudi nyuma
Mi n'na kisebusebu

Ni zabibu, utamu kuliko nyama
Na twabibu, anitulize mtima
Kwa adabu, nisinene ni lazima
Mi n'na kisebusebu

Ni kurabu, kulilea nishakoma
La kudabu, lafanya nishike tama
Sina jibu, nilipo nimechotama

Mi n'na kisebusebu

Usulubu, ni vyema anganinyima
Ni swahibu, kumuwata sio vyema
Ningatubu, ila sina la kusema
Mi n'na kisebusebu

Si adhabu, kujitweka wima wima
Na ya babu, kuyavunda ni ulema
Sio tabu, mwishoni kunisukuma
Mi n'na kisebusebu

Ukaribu, na mwisho hapa nakoma
Ni wajibu, ya moyoni kuyatema
Si haribu, japo pamekosa wema
Mi n'na kisebusebu

JITUZI

Haiwi kuwa jamali, kutoshukuru

Mwenyezi

Naandika kwa dalili, msinichambe upuzi

Msinikate kauli, mtanishusha mafuzi

Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

Mpishi mapishi ghali, anaiwezea kazi

Ulipika kwa ukweli, akalikoleza nazi

Vingojongojo usuli, nilifurure kwa pozi

Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

Thuzi hunipa morali, kulitema mi siwezi

Tena huwa ni shughuli, kulikomba silisazi

Wala vyanda havifeli, kulikombereza
thuzi

Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

Igwiyezi sawa ngeli, si kithuzi ni jituzi

Lanipagawisha nguli, msambe hawa bitozi

Kuimba taimba Ali, mana shaanza miluzi

Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

Rigo rigo thuzi tuli, mapishi ya ki uswazi
Sijaona sampuli, heri niliweke wazi
Linanishibisha hali, kwa raha namwaga
chozi
Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

Si mtana si laili, halitonipa ajizi
Nakowa tangu awali, si thuzi la utatizi
Laninenepesha mwili, hili wazi mumaizi
Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli

Tamati hapa muhali, nisambwe ni
mchochezi
Kutuwa ni afadhali, mbele katu siongezi
Thuzi menogesha Ali, limenitia uchizi
Kwayo tamu ya jituzi, sichi kuramba
bakuli!

TISHALI

Imenikumba shughuli, pevu
yakunitingisha
Limenisibu zohali, nahisi nimeshakwisha
Napapatika rijali, haya yaniogopesha
Tishali lanizamisha!!

Nilijikaza msuli, tishali kuliwezesha
Nikajizatiti Ali, fumbati kuziungisha
Kwa hali pia na mali, upyawe nikaregesha
Tishali lanizamisha!!

Nililiamini kweli, uzio litavukisha
Nikaiona dalili, ng'ambo litanifikisha
Leo hii ni badali, mudiri lanihizisha
Tishali lanizamisha!!

Lilivyo tishali hili, nilijua hapa tosha
Na kwa wangu ujahili, kasia nikazirusha
Sasa nakosa mwahali, wapi pakusalimisha
Tishali lanizamisha!!

Silo bovu li jalili, kwa nilivyo ling'arisha

Kwa vyuma vilivyo ghali, na rangi za
kuridhisha
Leo lanibwaga chali, juu juu lahemesha
Tishali lanizamisha!!

Wakokoni mtaali, tishali lisinifisha
Mana nakosa akili, imenipanda puresha
Macho tong'o ja mdoli, tayari
lishanichosha
Tishali lanizamisha!!

Forodhani nako mbali, hali yanisikitisha
Maili kumi na mbili, na pumzi zimenisha
Ningalijua awali, nisingelijidandisha
Tishali lanizamisha!!

Nane tama mi nakuli, funzo
limenifundisha
Sitojipa idhilali, daima tajikumbusha
Sitoamini tishali, mbele likanizamisha
Tishali lanizamisha!!

NGULENGULE

Naanda msi majuto, ziumbe nipulikani
Yeo nipulikanito, mnisikile makini
Nandikayo si matoto, nyute tafakari hini
Ya ngulengule tumboye!

Si maana ya malambi, niuzwe 'mbwa
nyani'
Siyaambi manenombi, kinikute kisirani
Yajuleni ya muambi, nduu zangu
shikaneni
Ya ngule ngule tumboye!

Utengano ni dhaifu, hayafutu duniani
Wangi waaze machafu, miji kuibwaga
zani
Yombo sio insafu, utaambwa limbukeni
Ya ngule ngule tumboye!

Naiga msikatili, Kiwandeo ufukweni
Ushindani wa wawili, mshindi hajulikani
Shikamano ni jamali, kondo mbaya
kilingeni
Ya ngule ngule tumboye!

Mataya yatakupwaya, unyapazi ni wa
nini!?
Siriyo ni siri mbaya, imi wanihusishani!?
Wawa mwivi ja ulaya, unavyaa ushetani!?
Ya ngule ngule tumboye!

Mawi Mudiri naiza, kheri ndo twaitakani
Ngule ngule yaumiza, hasa kwetu tulo
chini
Ndwisi inotutatiza, ikatuwacha tu duni
Ya ngule ngule tumboye!

Sitoiweka nadhiri, nishindwe niwe
dhambini
Ikikauka bahari, w avuvi mtavuwani
Na walimao ndodori, nguwe kangia
shambani
Ya ngule ngule tumboye!

Msambe hini mefumba, wafumbuzi
tokezeni
Kama wimbo ningaimba, mjuweto
mendikani

Mpingaji angelumba, malumbano
kilumbani
Ya ngule ngule tumboye

Mwisho salamu za Dotto, Ahmadi, Sufiani
Japo tungo ya kitoto, ni vyema
mukaighani
Hii imekuwa ndoto, ngule ngule yanikhini
Ya ngule ngule tumboye!

VINYAGO

Tungo hii kuitunga, imenikosha mdigo
Sio hoja mukajenga, mnikosowe vigogo
Simi mjuzi wa kunga, msinilambe kisogo
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Mkone lifata Tanga, nikenda kata kigogo
Nikanowa langu panga, yakiwa wazi
magego
Kwa mchongo wa shiranga, nikavichonga
vinyago
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Kavilaza langa langa, nakuchachaga
chachago
Visofaa kuvienga, sikulitaka sisigo
Kwa mfano wa puyanga, imi nalihisi zogo
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Nawa navishunga shunga, nikiwa mchama
ago

Nikionwa babu jinga, kuvitoroka vinyago
Hadi najiona bunga, jaye mshikwa wa
tego
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Mtetemo wanizonga, nalegeo limi fogo
Nongwa imeshaninanga, natitia mtitigo
Hatwari nishavichonga, na vivyo vyanipa
bwago
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Chembembe kinavyodunga, mtima wazidi
pigo
Mato nayo chenga chenga, ozi lilegeo lego
Siwezi tena kuringa, yananikakama mago
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Sogea Mwana wa Kanga, tatua niliyo nago
Mwenzio natanga tanga, tuli siipigi nyago
Akili meniboronga, hadi zaiuma figo

Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

Tamati yatimu kunga, nahitimisha mdigo
Mikono ninailinga, nawaachia vigogo
Heri nikashona shanga, vishanishinda
vinyago
Vyanitishia vinyago, mwenyewe
nilivyochonga

MWENDA KO

Sichi kubwaga andiko, n'kakisuta kijaro
Ile yao mihemko, naona waisha ngoro
Walivamiavyo soko, ngangari kumbe si
doro
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Watapata fadhaiko, nyuso ziwajae soro
Yao mawi matamko, kwangu siyatii njaro
Waendako mimi niko, ila hakufiki nyoro
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Wapayuka mipayuko, kwenye na kiza
totoro
Kucharuka micharuko, watimkavyo mairo
Watabaki macho soko, mwisho
wazishushe ndiro
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Watapatapa waliko, gugumizi la umiro
Hawana hadhi wanoko, pa kumi nawapa
ziro
Langu silo lao fuko, la daima kuwa, churo
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Ninawaonya vituko, msafara wao kero
Wasifia baikoko, goma la kisharobaru
Waucheza mdundiko, kuiga ngoma ya
ndaro
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Mbali hawafiki huko, hata watupwe kwa
tero
Hiyo yao miondoko, kwangu ishawa
kiporo
Wajuwe huku niliko, sio kwenye vigodoro
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

Sabaa tama andiko, leo sileti kokoro
Daima kumwamba duko, rangi kupaka
nguchiro
Ikiwa jambo si lako, basi wata ukachero
Wafwatavyo matotoro, hawatafika
wendako!

BALAA

Balaa niitungeto, utungo usende yombo
Silo fumbo nifumbeto, wala siandiki
wimbo
Na hayano si matoto, yalishangaza
kitambo
Iweje wanuka shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa roho ya kito, kisa wajuwa kimombo
Yawavyo haya mapito, punguza vimambo
mambo
'Ngawa umeng'aza mato, hujawa na njema
nembo
Kwa vipi unuke shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa ni upereto, nayo mangi majigambo
Watufyata fyoto fyoto, tangu ujulishwe
ng'ambo
Ila pii'yo Goroto, wanuka kwayo
michambo
Yawaje unuke shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa ya tumbo joto, walewa hujanwa
tembo
Limbukeni wa vipato, vyasinya vyako
vikumbo
Aibuzo nzito nzito, zitakupwaisha tumbo
Linakunukaje shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa ndo wako wito, uumbuwavyo
maumbo
Wavienzi vigogoto, kutulongeya mafumbo
Lisikughururi pato, haliwi ni jema jambo
Mbona likunuke shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa huwa majuto, mjitwika miserembo
Wajipoteza mvuto, kuringa kwako
m'vumbo
Keleti uliwazeto, isije kuvimba tambo
Kwa nini unuke shombo, muuzaji
manukato!?

Balaa hii si ndoto, rekebisha kenya kimbo
Ndo mwisho wangu Masito, simi mzengea
ndembo
Tuuzie manukato, nawe usinuke shombo
Hivi wanukaje shombo, muuzaji
manukato!?

BAKULI

Bisimika ya Jalali, Mola wangu ya Mlezi
Naandika lilo kweli, liloshuhudia ozi
Sipanii ya badali, naliweka hili wazi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Fikira zisende mbali, udhani nyama ya
mbuzi
Ukanikata kauli, bakuli tele mkizi
Utaonwa u jahili, kadhalika na upuzi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Sijajitia shughuli, nambwe himi
mchunguzi
Yawavyo yano muhali, sitofurura mchuzi
Nawafahamisha Ali, lisiwafike tatizi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Simi mjuzi si nguli, ila hili sigeuzi
Sijaoma sampuli, lachuruzika churuzi
Yashasinya mankuli, msambe imi bazazi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Heri ukapika sheli, ama rojo la viazi
Itakua ni sahali, kujipunguzia kazi
Halinayo afadhali, limbwa limbwa la
mchuzi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Sambi liwape zohali, mukaishi ki Bitozi
La buli ni buli buli, si hili ki chizi chizi
Litadobeza mahali, tafya tafya ya mchuzi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Tamaa wekeni mbali, msijekuwa mabozi
Hili si kwamba na bali, shikeni utambulizi
Lisijewalaza chali, ni bakuli la uswazi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

Majagina m'taali, mje nao ufumbuzi
Yaani bakuli hili, si nyama litele chuzi
Teja napakaa tuli, memaliza uchambuzi
Lilivyo tele bakuli, sio nyama ni mchuzi

BAHARI

Nitungile msi shari, nisingaonywa foriti
N'ja nilongile kheri, mbee siwe yalaiti
Tuliidhani shuwari, joshi hatukuzatiti
Imekatika shariti, ichafusie bahari!

Heri ngeabiri hori, tungaweza lidhibiti
Ishaangua hayari, demani siitefuti
Wa omo metahayari, na wa tezi hatunyuti
Imekatika shariti, ichafusie bahari!

Ilotuka ni hatwari, kinani tu katikati
Beta haina uzuri, mepasuka mlingoti
Kwa hini iiliyojiri, kupona ima bahati
Imekatika shariti, ichafusie bahari!

Wimbi deki sio siri, latitiza chombo titi
Imetutoka jeuri, sute tuambacha mbati
Baharia mjasiri, ila leo hatufiti
Imekatika shariti, ichafusie bahari!

Hawavuliki jodari, imeshaachia neti
Yowe ja wapiga twari, afuweni hatupati
Tusubiriyo athari, kifo cha wengi ni pati

Imekatika shariti, ichafusie bahari!!

Mambo kikiri kikiri, mwisho hapa ni
tamati

Ishachafuka bahari, twasubiri mkiriti
Bohari hii bohari, naliangukia goti
Imekatika shariti, ichafusie bahari!

HAKIOMBWI

Utungo ningekaanga, kama fumbo
halifumbwi
Kunga naivungavunga, isije kuwa
masumbwi
Vina nisivyo vipanga, Tena sitaki
uchambwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Walevi warengarenga, kwao wema
hawagombwi
Tena wanavyo singanga, sifa zao
hazipambwi
Wajibwage langa langa, hili katu
haliombwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Makahaba wanatanga, hawahofu lambwi
lambwi
Na pia kuwasimanga, utowaamba li
ambwi

Dua mutake zipanga, hamutawachimba
chimbwi

Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Na wale wavuta unga, wanavyodimbwika
dimbwi

Roho kuwatangatanga, wamezowea
mavimbwi

Iwapo walijitenga, dua hii hawapambwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Safu safu twajipanga, kutogeuka ja
lumbwi

Maombi tukiyalenga, kwako aloumba
numbwi

Kuomba hili majanga, tutaonekana
zimbwi

Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Dunia kono kipunga, nao ubaya siimbwi
Sifa tele nitajenga, na nongo mbaya
sigombwi
Kuniombea Malenga, ila hilo haliombwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Wajuzi wa hizi kunga, kipi eti hakiombwi
Mizani vina kupanga, fumbueni
kiufumbwi
Nimelipandisha tanga, usije zama
mtumbwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

Nahitimisha kutunga, Teja na shari
sigombwi
Ingawa simi malenga, sitembweki tembwi
tembwi
Yuwapi alie lenga, kunijibu mi silembwi
Ndicho hicho hakiombwi, hata kwa walio
wanga

KIATU

Sawazisha, tusitete, usininadi vibaya
Sitobisha, na nijute, nikajikondea taya
Rekebisha, usibete, ya kuambiwa sikiya
Wakivisha, watu wote, lazima
kitakupwaya!

Nakumbusha, tema mate, isiwe nakuzuliya
Ungabisha, mi nisite, huko sikusaidiya
Aminisha, jikukute, ufate ilo sawiya
Ushavisha, watu wote, ni sawa
kikikupwaya!

Wachekesha, unisute, eti nakuharibiya
Kunitisha, siku zote, na yangu
yaniendeya
Badilisha, yako kete, ima sivyo wapoteya
Kukivisha, watu wote, ona kinavyo
kupwaya!

Watingisha, guu lote, kiweze kumuingiya
Tamausha, nacho chote, hakina pakuzuiya
Kishakwisha, kote kote, huwezi
kukiringiya

Kuwavisha, watu wote, ndiposa
kimekupwaya!

Kuzungusha, nchi yote, ndo
kulikuharibiya
Waridhisha, kila pote, kipi ulitegemeya!
Sasa bisha, na yeyote, kama hatokichukiya
Ulivisha, watu wote, na sasa
kinakupwaya!

Tamatisha, nisisote, kiatu nakuachiya
Na bashasha, ipopote, wala sitokirudiya
Imetosha, usinyete, kipyaa najinunuliya
Kwa kuvisha, watu wote, iweje
kisikupwaya!

CHAKA

Sajida yake Moliwa, mie namsujudia
Kisha najiweka sawa, tayari kuwandikia
Haiwi haiwi huwa, ila si njema twabia
Chaka litele malaji, mbona simba ale
simba!?

Laana imekithiri, chaka mengia udhia
Si kwa siri si dhahiri, uovu kutufikia
Inapaliliwa shari, huluka yawafifia
Chaka mezagaa mlo, fisi amlaje fisi!?

Vitoria na ubuyu, chakani vinanyinyia
Huyu hamtaki huyu, madhuluma mia mia
Si la Pate si la Siyu, wapembe hana mkia
Chaka furi furi shibe, nyati atafuna nyati!?

Hufanya maandamano, iwatunuku sharia
Migomo na minong'ono, eti njia kujilia
Hata nao konokono, aibu wanajitia
Chaka mejaa vyakula, ngiri amlaje ngiri!?

Imeozea shuruti, ngwee yasikitikia
Yawa ya kaumu luti, walanivyo jumuia

Dhambi malipo mauti, mwituni kiungulia
Chaka lisilo na njaa, chatu ammize chatu!?

Li ovyo chaka li ovyo, paa wataka kimbia
Hali moto yawa vivyo, nguruwe
wanaumia
Yazidipo vivyo hivyo, msitu wadidimia
Chaka mejaa mapocho, chui akwaruza
chui!?

Lanijaa sikitiko, huzuni hadi nalia
Tuendako huko siko, ghururi hii dunia
Ya boko kumla boko, Mungu atatununia
Chaka vyakula pomoni, nyani pia ale
nyani!?

Mwisho dua kwa Manani, kheri tunaitakia
Atulinde duniani, gharika situfikia
Yanotutweza chakani, wayaalamu Rabia
Chaka litele wanyama, mtu amlaje mtu!?

SI MIMI

Si mimi naiandika, Mola amenijalia
Si mimi nitasikika, ijuwe hili dunia
Si mimi mkhasirika, katu siwezi fulia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi sitoki nyika, huko uliko kulia
Si mimi wa kuumbuka, vii wakuvirukia
Si mimi sitoumbuka, hili wazi nakwambia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi tena hakika, siye wakukurudia
Si mimi si lako rika, hunifai nisikia
Si mimi nisharidhika, nilipo nimetulia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi ninakucheka, haswa kwa ulivyo
via
Si mimi kwa yalo tuka, niwe Teja
maridhia
Si mimi naapa fika, huna la kunifanyia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi wa pata shika, roho yangu najulia
Si mimi sitoropoka, kama weye njia njia
Si mimi mnusurika, aibu ulonitia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi wakukusaka, uje unipe udhia
Si mimi wakukutaka, ndwele uje nipatia
Si mimi nisharidhika, anipenda mai dia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi wa zama zuka, watsapu
kukuchatia
Si mimi nimekutoka, mesenja na imo pia
Si mimi nishakuchoka, aise nakuchukia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

Si mimi ni ya Rabbuka, haya alonijalia
Si mimi huu mzuka, huna pakuingilia
Si mimi ya tamatika, jumbe imekufikia
Si mimi wakubukia, tapishi nilotapika!

NAANZAJE

Naanzaje kukufuru, nisimshukuru Mola!?

Naanzaje mwenye kwiru, nikisusie
chakula!?

Naanzaje na udhuru, nikauwacha mswala?

Naanzaje kujidunga, nikarudi utejani!?

Naanzaje msi ndonga, nikakesha
kilingeni!?

Naanzaje kuyatunga, kumbe sihiyisi fani!?

Naanzaje kumcheka, mja aliye na
ndwele!?

Naanzaje kuropoka, kukataliwa ki vile!?

Naanzaje pata shika, kiwadharau
wavyele!?

Naanzaje kumsuta, nilompa unafiki!?

Naanzaje navyo vita, nikampiga rafiki!?

Naanzaje nayo nguta, nikiteta haisuki!?

Naanzaje kwenda posa, mrembo
sijamuona!?
Naanzaje nna pesa, ila nife kiutwana!?
Naanzaje kupepesa, na pa mana nshaona!?

Naanzaje mi kuchati, kisimu cha totoriro!?
Naanzaje nikabeti, mfukoni nna ziro!?
Naanzaje afiriti, kukubali zake kero!?

Naanzaje tungo hino, mwisho
nisipaandike!?
Naanzaje huno wino, ya kwamba
usisomeke
Naanzaje msumeno, kikatwa nisikatike!?

NASHUKURU

Sicheki nikiandika, Mungu alonijaliya
Mana sijakamilika, mja huikosa ndiya
Kwa vivi nitasomeka, kwayo ninayo
longeya
Nashukuru kila mara, sicheki alo kilema!

Sicheki alo kilema, niambe hajatimiya
Kwa kuwa haendi wima, nikamdharauliya
Nikujitwika lawama, na Mola kumkoseya!
Nashukuru kila mara, sicheki alo na
ndwele!

Sicheki alo na ndwele, ukimwi na
malariya
Nikamguna kwa lile, analo liuguliya
Kwao mtihani ule, ni dua kumuombeya
Nashukuru kila mara, sicheki mvuta unga!

Sicheki mvuta unga, sigara na bangi piya
Na siwaoni wajinga, kwa kuwa niliachiya
Ni imani kuwajenga, hwenda
wakazingatiya
Nashukuru kila mara, sicheki alo fukara!

Sicheki alo fukara, masikini wa duniya
Hilo Allah lamkera, keshakemea Nabiya
Hini dunia duwara, yasije kunirudiya
Nashukuru kila mara, sicheki aso elimu!

Sicheki aso elimu, hila nikampatiya
Nahisi ni kudhulumu, neema zakwe Jaliya
Sitojifanya mwalimu, aso juwa kukemeya
Nashukuru kila mara, sicheki aso na mke!

Sicheki aso na mke, huko nikujitongeya
Kwangu talaka itoke, niwe ninachiyachiya
Sifanyi asononeke, ndoa doa akatiya
Nashukuru kila mara, sicheki mtunga
shombo!

Sicheki mtunga shombo, tungo
nikimaliziya
Sitafanya majigambo, Mola wangu
nepushiya
Nisichukie ya yombo, na yangu nikasifiya
Nashukuru kila mara, sicheki nikakufuru!

DOLE

Kwa jina lake Moliwa, Mungu wa kale na
kale

Wa enzi ano sifiwa, wa milele na milele
Leo nataka sikiwa, furaha nnayo tele
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

Si wazimu nipo sawa, siropoki hili lile
Ima ni yangu ngekewa, kumvunda chawa
yule
Sio pauka pakawa, limeweza hili dole
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

Jichawa kubwa kishuwa, sikufanyia simile
Na damu nikalitowa, bila hata ukelele
Nguvu sikupungukiwa, nikalifinya kwa
mbele
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

Kweli nimelipasua, kalivuruja umbole
Silo la kusingiziwa, nije makwa asalale
Amini sikuchelewa, nikalibania pale
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

Melipenduwa penduwa, limuradi
linyamale
Kwa makini likatuwa, nikalipeleka dole
Sauti halikutowa, nipozika dole lile
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

Msinipimie hewa, mwambe napinga
wavyele
Nimeweza naelewa, si yale ya ngule ngule
Leo ninakutuwa, naamini langu dole
Moja hili langu dole, leo limevunja
chawa!!

HAMUYO

Menibid niandike, si kiburi, na Wala sio
uhuni
Na sitaki nikucheke, si ushahi, unichukie
moyoni
Nalo hili lipulike, si hiyari, ndo habari ya
mjinii
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Hata nawe urauke, sio siri, wazo lako
kwangu duni
Nayasema maanake, si vizuri, unitie
lawamani
Uanguke unyanyuke, si hatari, yako
hayamo kichwani
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Sijilete kwa makeke, kijasiri, wala
hutoona ndani
Kama kufoka ufoke, kihodari, na bado
najiadini

Uamuzi si geuke, jemedari, nitayari kwayo
nduni
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Sitokufanya udeke, eti zari, utangaze
tandaoni
Na haiwi mwake mwake, furi furi, heri
nilibebe zani
Teseke na uteseke, nyiri nyiri, ninalo
langu likani
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Hata uongee peke, siwi chori, nijitie
kitanzini
Ubayao uroweke, machachari, mie sitoona
soni
Kujisweka we jisweke, kama shari,
atahukumu Manani
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Nakunyoosha unyoke, ndio kheri,
ujekumbuka mbeleni
Tulia sibabaike, na ndunguri,
tushazikwepa zamani
Ima we ubadilike, kwa uzuri, sikuwachi
matesoni
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

Tama mwisho niandike, ndo akhiri, shairi
hili mwishoni
Somo Teja nisomeke, na shairi, ulitie
akilini
Hamuyo ndugu iweke, tahadhari,
siumbuke kilingeni
Simchinji ng'ombe wangu, kwa hamuyo
ya maini!

UTAPOKEAJE

Ghafula yani ghafula, anitwae Mola
wangu

Kuamka na kulala, yenezwe tanzia yangu
Ikisambaa risala, kuuaga ulimwengu
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu?

Mfaume Ulamaa, mtafanyaje wenzangu?
Ngonjera itanifaa, au dua kwake Mungu?
Au mutawashangaa, kubadili jina langu?
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu?

Utakuwaje Alma, utamiss jumbe zangu?
Yani utashika tama, na kutazama mawingu
Hutaamini nasema, ndivyo nishaenda
vyangu
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu!?

Ewe mwana wa Chitsangi, utauhisi
uchungu!?
Ulie machozi mengi, na uje joshoni
pangu!?
Utavikumbuka vingi, nakuhisi pengo
kwangu?

Hivi utapokeaje, habari za kifo changu?

Mtalia wana samba, Mwachausa kaka
yangu?

Kwa huzuni mutaimba, muwajuze
walimwengu?

Likitoweka dzagamba, utawajaa ukungu?
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu!

Picha zangu fesibuku, zikitanda kama
wingu

Sharifa utajishuku, kutamani yetu pingu
Mjuwe siwekwi mwiku, wasia wangu wa
tangu

Hivi utapokeaje, habari za kifo changu!

Watawapigia simu, jamaa aali zangu
Zitawatia wazimu, muhisi kizunguzungu
Ila fika mfahamu, litakuwa langu fungu
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu!

Tama ya tama tamati, namuomba Mungu
wangu
Khatima njema mauti, hino ndio dua
yangu
Mudiri natia hati, nifapo ridhia Mungu
Hivi utapokeaje, habari za kifo changu!

DUA

Naomba nibarikiwe, neema ziongezeke
Maombi niitikiwe, niombalo lifanyike
Liso na kheri lisiwe, madhila yasinifike
Daima nihifadhike

Naomba nifanikiwe, na moyo ufurahike
Maovu niepushiwe, madhila yaniepuke
Kwa uzuri nisifiwe, vibaya nisitajike
Kwa Mola nisitirike

Naomba nikusanyiwe, wazuri
wanizunguke
Milango nifunguliwe, hadhi yangu itukuke
Wabaya niepushiwe, shari zao niepuke
Na nyuma nisizunguke

Naomba nijaaliwe, hisani niikumbuke
Lolote lile naliwe, mwenzangu nisimruke
Mwizi kwa hilo nisiwe, si vizuri
tukumbuke
Milele nisigeuke

Naomba niafiqiwe, ibada nikazishike

Mwenye riyaa nisiwe, ikhlaswi nijitwike
Ili peponi nitiwe, na mimi nipumzike
Du'a yangu isikike

Naomba akaafiwe, mgonjwa asishikike
Uzima arudishiwe, na sote tufurahike
Na nguvu azidishiwe, ibada zikamilike
Wapendwa wanusurike

Thank you for choosing
DESTINY INK PUBLISHERS LTD

EMAIL:

destinyinkpublishers@gmail.com

+254756652525 / +254758966662

+254114834135 / +254114581038

For

1. Book edition
2. Book translation.
3. All designs
4. Branding
5. ISBN issuance.
6. Copyright.
7. Printing.
8. Marketing.
9. Social media handling.
10. Book layout
11. Writing coaching.
12. Digital publishing.